

UKATILI WA MRENO

HABARI tulizozipokea zasema kuwa vitendo vya Wareno katika Msumbiji ni kuendesha upelelezi (PIDE) baada ya kuruhusiwa na Serkali hiyo, kuwa na International Police of Defence of States wapatao 25, na kati ya hao sita wako mjini Sulisbury.

Manuel Maangate, PIDE aliyeajiriwa na Jameson Hoteli mjini Sulisbury ametumwa Beira akijifanya mfungwa ili kutoa majina ya wanachama wa Portuguese East Africa Society ambacho kina ruhusa kuendesha mambo yake katika Rhodesia ya Kusini, kwa Serkali ya Wareno, na wanachama wa chache huko Harare wanasakwa na kukamatwa na kurudishwa Mozambiki.

Atakuja Dar

Ujumbe mwingine wa Manuel ni kuja Dar es-Salaam kutafuta habari na mambo ya FRELIMO na kutoa kwa Wareno. Amekwisha watulisha wakimbizi wa Mozambiki juu ya kuja kwake.

Bwana Neves anayefanya kazi katika Utawala huko Beira amepewa kazi aende Sulisbury kila Jumatano kwenda kuwaiba au kuwakama'a wanasiasa wananchi wa Mozambiki watiliwao shaka na kuwafunga kwenye magereza nchini huko. Kazi chafu ya ukatili hufanywa wakati wa usiku kwa mapatano na Serkali ya Rhodesia ya Kusini.

Maalamiko UNO

Kwa kuuata matakwa ya Pafmeca katika mkutano wake wa Leopoldville Desemba 28-31 chama cha Frelimo kiliwakilishwa na Rais Mdogo Bwana Uria T. Simanor. Mkutano huo aliazidi kupeleka malalamiko makali sana kwenye Umoja wa Mataifa ili Wareno waache kuni awa la Mozambiki na nchi zingine wanazozitawala katika Afrika mwaka huu 1963. Na kama Ureno haitaki, Pafmeca na nchi zingine za Kiafrika zingeingilia jambo hilo.

Wasome Uku'ani

Wareno wanawati-hia na kuwakatili vibaya

wananchi wanapigania uhuru wao. Kitendo kama hicho kinawafanya wananchi wawe wanadai uhuru wao kwa vurugu na ghasia. Chama cha Frelimo kinawa uliza Wareno kusoma ukutani mlimoandikwa ta

rehe ya uhuru wa Mozambiki. Kwa sababu ya ugumu wa Wareno Chama kilijadili kwenye mkutano wake wa Septemba 1963 maonyo kama haya; "Frelimo haihusiki katika hasara ya vifo na mali ambayo imeletwa na Wareno na mambo yake ni maangamizo ambayo Serkali ya Wareno sasa ina ishuhu lishha na kuyafanya kati ya Wareno na watu wa Mozambiki.